- 23 When they persecute you in one town, flee to the next; for truly I tell you, you will not have gone through all the towns of Israel before the Son of Man comes.

**UV**

- 23 Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu.

**NT Zanzibar**

- 23 Watakapowaudhi katika mji huu, kimbilieni mwingine: kwa maana ni kweli nawaambieni, Hamtaimaliza miji yote ya Israeli, hatta ajapo Mwana wa Adamu.

**NT Mombasa**

- 23 Nao watakapowaudhi katika mji huu, ukimbilieni mwingine; kwani ni kweli nawambia, hamtaimiza miji ya Israeli, illa atakuja yule Mwana wa bin-Adamu.

**Roehl**

- 23 Lakini watakapowafukuza mjini humu, kimbilieni mwingine! Kwani nawaambiani iliyo kweli: Hamtaimaliza miji ya Israeli, mpaka Mwana wa mtu atakapokuja.

**Habari Njema**

- 23 “Watu wakiwadhulumu katika mji mmoja, kimbilieni mji mwingine. Kweli nawaambieni, hamtamaliza ziara yenu katika miji yote ya Israeli kabla Mwana wa Mtu hajafika.

**Neno**

- 23 Wakiwatesa katika mji mmoja, kimbilieni mji mwingine. Kwa maana nawaambieni hakika, hamtamaliza kuipitia miji yote ya Israeli kabla Mwana wa Adamu hajafika.

**Matthew 15:21-28**

**NRSV**

- 21 Jesus left that place and went away to the district of Tyre and Sidon.  
22 Just then a Canaanite woman from that region came out and started shouting, "Have mercy on me, Lord, Son of David; my daughter is tormented by a demon."  
23 But he did not answer her at all. And his disciples came and urged him, saying, "Send her away, for she keeps shouting after us."  
24 He answered, "I was sent only to the lost sheep of the house of Israel."  
25 But she came and knelt before him, saying, "Lord, help me."  
26 He answered, "It is not fair to take the children's food and throw it to the dogs."  
27 She said, "Yes, Lord, yet even the dogs eat the crumbs that fall from their masters' table."  
28 Then Jesus answered her, "Woman, great is your faith! Let it be done for you as you wish." And her daughter was healed instantly.

**UV**

- 21 Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.  
22 Na tazama, mwanamke Mkananayo [Mkanaani] wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.  
23 Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele [kwa kuwa anaendelea kutupigia makelele] nyuma yetu.  
24 Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.  
25 Naye akaja akamsujudia, akisema Bwana, unisaidie.  
26 Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.  
27 Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.  
28 Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

**NT Zanzibar**

- 21 Yesu akatoka huko, akaenda pande za Turo na Sidon.  
22 Na mwanamke Mkananaya wa mipaka ile akatokea, akampaazia sauti, akinena, yangu Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daud; binti yangu amepagawa sana na pepo.  
23 Nae hakumjibu neno. Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakinena, Mwache aende zake; kwa maana anapiga nyuma yetu.  
24 Nae akajibu, akasema, Sikupelekwa illa kwa kondoo zilizopotea za nyumba ya Israeli.  
25 Nae akaja akamsujudia, akinena, Bwana, nisaidie.  
26 Akajibu akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.  
27 Akasema, Ndio, Bwana, illakini hatta mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.  
28 Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Ee mwanamke, imani yako kubwa; pata utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

## **NT Mombasa**

- 22 Nae, huyo ndiye, mwanamke wa Kikanani, nae ni mtu wa katika mipaka ile, akatokea akapiga kelele, yuana, Nirehemu Bwana, Mwana wa Daudi; binti wangu yuateswa sana ni pepo.
- 23 Asimjibu neno. Wakamwendea wanafunzi wakwe wakamsihi, wanena, Mpe rukhusa mwanamke, kwa kuwa atufuata huku akitupigia kelele.
- 24 Akajibu akanena, Sikutumwa illa kwa kondoo wapotevu wa nyumba ya Isiraeli.
- 25 Nae mwanamke akamwendea, ikawa kumsujudia, yuana, bwana, nisaidia.
- 26 Akajibu akamwambia, Si vyema kuutwaa mkate wao wana kuwatupia mbwa.
- 27 Akanena, Ndiyo Bwana, kwani hata mbwa hula katika makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.
- 28 Ndipo hapo Jesu akamjibu akamwambia, Ewe mwanamke, imani yako ni kubwa: na yawe kwako kama utakayo. Akapoa binti wakwe kwa saa ile.

## **Roehl**

- 21 Yesu alipotoka huko akajiepusha kwenda pande za Tiro na Sidoni.
- 22 Mara mwanamke wa Kikanaani aliyekaa mipakani huko akatokea, akapaza sauti akisema: Nihurumie, Bwana, mwana wa Dawidi! Binti yangu anapagawa vibaya na pepo.
- 23 Lakini hakumjibu neno. Wanafunzi wake wakamjia, wakamwomba wakisema: Mwache, aende zake! Kwani anatupigia kelele nyuma yetu.
- 24 Naye akajibu: Sikutumwa pengine, ni kwao tu walio kondoo waliopotea wa mlango wa Isiraeli.
- 25 Naye mwanamke akaja, akamwangukia, akasema: Bwana, nisaidie!
- 26 Naye akajibu akisema: Haifai kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia vijibwa.
- 27 Mwanamke akasema: Ndio Bwana, lakini nao vijibwa hula makombo yanayoanguka mezani pa bwana zao.
- 28 Ndipo, Yesu, alipojibu akimwambia: Mama, umenitegemea kabisa. Na uvipate unavyovitaka! Saa ileile binti yake akapona.

## **Habari Njema**

- 21 Yesu aliondoka mahali hapo akaenda kukaa katika sehemu za Tiro na Sidoni.
- 22 Basi, mama mmoja Mkanaani wa nchi hiyo alimjia, akapaaza sauti: “Bwana, Mwana wa Daudi, nionee huruma! Binti yangu anasumbuliwa na pepo.”
- 23 Lakini Yesu hakumjibu neno. Basi wanafunzi wake wakamwendea, wakamwambia, “Mwambie aende zake kwa maana anatufuatafuata akipiga kelele.”
- 24 Yesu akajibu, “Sikutumwa ila kwa watu wa Israeli waliopotea kama kondoo.”
- 25 Hapo huyo mama akaja, akamsujudia, akasema, “Bwana, nisaidie.”
- 26 Yesu akajibu, “Si vizuri kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.”
- 27 Huyo mama akajibu, “Ni kweli, Bwana; lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka mesa ya bwana wao.”
- 28 Hapo Yesu akamjibu, “Mama, imani yako ni kubwa; basi, ufanyiwe kama unavyotaka.” Yule binti yake akapona wakati huohuo.

**Neno**

- 21 Na Yesu akaondoka mahali hapo akaenda sehemu za Tiro na Sidoni.
- 22 Mwanamke mmoja Mkanaani aliyeishi sehemu hizo akaja kwake, akamlilia, akasema, “Nihurimie, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa na pepo na anasumbua sana.”
- 23 Lakini Yesu halumjibu neno. Basi wanafunzi wake wakamwendea wakamwomba, “Mwambie aende zake, kwa maana anaendelea kutupigia kelele.”
- 24 Akajibu, “Nimetumwa tu kwa ajili ya kondoo wa Israeli waliopotea.”
- 25 Lakini yule mwanamke akaja, akapiga magoti mbele ya Yesu akasema, “Bwana, nisaidie!”
- 26 Yesu akajibu, “Si haki kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.”
- 27 Yule mwanamke akajibu, “Ndio, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka kwenye mesa za mabwana wao.”
- 28 Ndipo Yesu akamwambia, “Mama, imani yako ni kubwa! Na ufanyiwe kama unavyotaka.” Tangu wakati huo mtoto wake akapona.

**John 1:18****NRSV**

- 18 No one has ever seen God. It is God the only Son, who is close to the Father's heart, who has made him known.

**UV**

- 18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.

**NT Zanzibar**

- 18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mwana wa pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyefasiri khabari yake.

**NT Mombasa**

- 18 Hakuna aliyemuona Mngu, popote; Mwana mzaliwa pekee, mwenyi kuwa katika kifua cha Baba, ndiye huyo aliyefunua.

**Roehl**

- 18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu hapo kale po pote, Mwana wa Mungu aliyezaliwa wa pekee, aliyeambatana na Baba, ndiye aliyetusimulia.

**Habari Njema**

- 18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote ule. Mwana wa pekee aliye Mungu ambaye ameungana na Baba, ndiye aliyetujulisha habari za Mungu.

**Neno**

- 18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote. Lakini Mwanac pekee, ambaye ana uhusiano wa karibu sana na Baba yake, amemdhahirisha Mungu kwetu.



**John 14:15-17, 25-26**

**NRSV**

- 15 “If you love me, you will keep my commandments.  
16 And I will ask the Father, and he will give you another Advocate, to be with you forever.  
17 This is the Spirit of truth, whom the world cannot receive, because it neither sees him nor knows him. You know him, because he abides with you, and he will be in you.
- 25 “I have said these things to you while I am still with you.  
26 But the Advocate, the Holy Spirit, whom the Father will send in my name, will teach you everything, and remind you of all that I have said to you.

**UV**

- 15 Mkinipenda, mtazishika amri zangu.  
16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;  
17 ndiye Roho wa kweli; ambaye uliwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.
- 25 Hayo ndiyo niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu.  
26 Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka [atamtuma] kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

**NT Zanzibar**

- 15 Mkinipenda, mtazishika amri zangu.  
16 Na mimi nitamwomba Baba, nae atawapa Mfariji mwingine, akaae nanyi hatta milele;  
17 Roho wa kweli; ambae uliwengu hauwezi kumkubali, kwa kuwa haumwoni wala haumjui; bali ninyi mnamjua, maana anakaa kwenu, nae atakuwa ndani yenu.
- 25 Haya nimewaambia, nikikaa kwenu.  
26 Lakini Mfariji, Roho Mtakatifu, ambae Baba atampeleka kwa jina langu, yeye atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

**NT Mombasa**

- 15 Mkinipenda mtayashika maagizo yangu.  
16 Nami tamtaka Baba, nae atawapa Msaada mwengine, apate kuwa pamoja nanywi milele,  
17 nae ni Roho wa kweli, ulimwengu usioweza kumtwaa, kwa kuwa haumuoni wala haumjui. Nyinywi mwamjua, kwa kuwa aketi kwenu, nae atakuwa ndani yenu.
- 25 *Maneno* haya nimewambia nili kwenu.  
26 Lakini yule Msaada, yule Roho Mtakatifu atakaeletwa ni Baba kwa jina langu, yeye atawafunza mambo yote, nae atawakumbusha niliyowambia yote.

### **Roehl**

- 15 Mkinipenda yashikeni maagizo yangu!
- 16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa mtuliza mioyo mwingine, akae pamoja nanyi kale na kale.
- 17 Ndiye Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sabbau haumwoni, wala haumtambui. Ninyi mnamtambua, kwani anakaa kwenu, naye atakuwamo mwenu.
- 25 Haya nimewaambia nikingali kwenu.
- 26 Lakini yule mtuliza mioyo, yule Roho Mtakatifu, Baba atakayemtuma katika Jina langu, ndiye atakayewafundisha yote na kuwakumbusha yote, mimi niliyowaambia ninyi.

### **Habari Njema**

- 15 “Mkinipenda mtazishika amri zangu.
- 16 Nami nitamwomba Baba naye atawapeni Msaidizi mwingine, atakayekaa nanyi milele.
- 17 Yeye ni Roho wa ukweli. Ulimwengu hauwezi kumpokea kwa sababu hauwezi kumwona wala kumjua. Lakini nyinyi mnamjua kwa sababu anabaki nanyi nay u ndani yenu.
- 25 “Nimewaambieni mambo haya nikiwa bado pamoja nanyi,
- 26 lakini Msaidizi, Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundishieni kila kitu na kuwakumbusheni yote niliyowaambieni.

### **Neno**

- 15 “Kama mnanipenda mtatimiza amri zangu.
- 16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapeni Msaidizi mwingine akae nanyi siku zote.
- 17 Huyu ndiye Roho wa Kweli ambaye watu wasioamini hawawezi kumpokea. Watu kama hao hawamwoni wala hawamfahamu. Ninyi mnamfahamu kwa kuwa anakaa ndani yenu na ataendelea kuwa nanyi.
- 25 “Nimewaambia mambo haya wakati nikiwa badi nipo nanyi.
- 26 Lakini yule Msaidizi, yaani Roho Mtakatifu, ambaye Baba yangu atamtuma kwenu kwa jina langu, atawafundisha mambo yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

**Acts of the Apostles 2:22-23, 36**

**NRSV**

- 22 “You that are Israelites, listen to what I have to say: Jesus of Nazareth, a man attested to you by God with deeds of power, wonders, and signs that God did through him among you, as you yourselves know –
- 23 this man, handed over to you according to the definite plan and foreknowledge of God, you crucified and killed by the hands of those outside the law.
- 36 Therefore let the entire house of Israel know with certainty that God has made him both Lord and Messiah, this Jesus whom you crucified.”

**UV**

- 22 Enyi waume [wanaume] wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;
- 23 mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua.
- 36 Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo.

**NT Zanzibar**

- 22 Enyi waume wa Israeli, sikieni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishiwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;
- 23 mtu huyu alitwaliwa nanyi kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, nanyi mkamsulubisha kwa mikono mibaya, mkamwua:
- 36 Bassi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo.

**NT Mombasa**

- 22 Enywi waume wa Isiraeli, sikizani maneno haya: Jesu Mnazari, mtu aliyedhihirishwa kwenu ni Mngu kwa vitendo vya nguvu, na vioja, na ishara, ambazo Mwenyiezi Mngu alizifanya katikati yenu kwa yeye, kama nyinywi wenyewe mjuavyo;
- 23 Yeye kwa shauri la Mngu lililoazimiwa na kwa kutangulia kujua kwakwe, nyinywi mmemsalibi na kumuua kwa mikono ya madhalimu:
- 36 Basi nyumba yote ya Isiraeli na ijue pasipokuwa na shaka, ya kwamba yeye Jesu mliyemsalibu myinywi Mwenyiezi Mngu amemfanya awe Bwana tena awe Masihi.

### **Roehl**

- 22 Enyi waume wa Kiisraeli, yasikilizeni maneno haya! Yesu wa Nasareti alikuwa amejulikana, kwamba ametoka kwa Mungu hapo, alipokuja kwenu na kufanya vya nguvu na vioja na vielekezo, tena ni Mungu aliyempa kuvifanya machoni penu, kama mnavyojua wenyewe.
- 23 Kwa kuwa Mungu alikuwa amempatia kazi na kumkatia mpaka kwa vile, anavyovijua vyote, vikiwa havijatimia bado, kwa hiyo ametolewa, mkampata mikononi mwa wapotovu, mkamwua na kumwamba msalabani.
- 36 Kwa hiyo wote walio wa mlango wa Isiraeli watambue kweli: Huyo Yesu, mliyemwamba msalabani ninyi, Mungu amemfanya, awe Bwana na Kristo!

### **Habari Njema**

- 22 “Wananchi wa Israeli, sikilizeni maneno haya! Yesu wa Nazareti alikuwa mtu ambaye mamlaka yake ya kimungu yalithibitishwa kwenu kwa miujiza, maajabu na ishara Mungu alizofanya kati yenu kwa njia yake, kama mnavyojua.
- 23 Kufuatana na mpango wake mwenyewe Mungu alikwisha amua kwamba Yesu angetiwa mikononi mwenu; nanyi mkamwua kwa kuwaachia watu wabaya kumsulubisha.
- 36 “Watu wote wa Israeli wanapaswa kufahamu kwa hakika kwamba huyo Yesu mliyemsulubisha, ndiye huyo ambaye Mungu amemfanya kwa Bwana na Kristo.”

### **Neno**

- 22 “Nawasihi ninyi Waisraeli mnisikilize. Yesu wa Nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa njia ya miujiza, maajabu na ishara, kama ninyi wneyewe mjuavayo.
- 23 Huyu Yesu alitiwa mikononi mwenu kwa mpango na makusudi ya Mungu aliyoyafahamu tangu awali. Nanyi mlimuwa kwa kumtundika na kumpigilia misumari msalabani, mkisaidiwa na watu waovu.
- 36 “Basi nataka niwahakikishie Waisraeli wote ya kuwa, Mungu amemfanya huyu Yesu ambaye ninyi mlimsulubisha, kuwa ndiye Bwana na Kristo.

### **Romans 3:19-25**

#### **NRSV**

- 19 Now we know that whatever the law says, it speaks to those who are under the law, so that every mouth may be silenced, and the whole world may be held accountable to God.
- 20 For “no human being will be justified in his sight” by deeds prescribed by the law, for through the law comes the knowledge of sin.
- 21 But now, irrespective of law, the righteousness of God has been disclosed, and is attested by the law and the prophets,
- 22 the righteousness of God through faith in Jesus Christ for all who believe. For there is no distinction,
- 23 since all have sinned and fall short of the glory of God;
- 24 they are now justified by his grace as a gift, through the redemption that is in Christ Jesus,
- 25 whom God put forward as a sacrifice of atonement by his blood, effective through faith. He did this to show his righteousness, because in his divine forbearance he had passed over the sins previously committed;

#### **UV**

- 19 Basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu;
- 20 kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.
- 21 Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii;
- 22 ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti;
- 23 kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;
- 24 wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;
- 25 ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe [aoneshe] haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa;

#### **NT Zanzibar**

- 19 Twajua ya kuwa mambo yote yasemwayo na torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, ulimwengu wote ukapasiwe na hukumu ya Mungu:
- 20 kwa maana hapana mwenye mwili atakayehesabiwa kuwa na haki mbele za Mungu, kwa matendo ya sheria: kwa maana kujua dhambi kabisa huja kwa njia ya sheria.
- 21 Sasa, lakini, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sharia, inashuhudiwa na torati na manabii,
- 22 ni haki ya Mungu, ipatwayo kwa kuwa na imani kwa Yesu Kristo, huja kwa watu wote, huwakalia watu wote waaminio.
- 23 Maana hapana tofauti; kwa sababu wote wamefanya dhambi, wanaona kwamba wamepungukiwa utukufu wa Mungu;
- 24 wanapewa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Yesu Kristo:
- 25 ambae Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa njia ya imani, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia dhambi zilizotangulia, katika uvumulivu wa Mungu:

## NT Mombasa

- 19 Twajua ya kwamba yale yote yasemwayo ni sharia, *sharia* huwambia wale tini ya sharia: illi kwamba killa kanwa lifumbwe na dunia nzima kuletwa katika hukumu ya Mwenyezi Mngu:
- 20 kwa maana, mbele yakwe hapana mwenyi muwili atakaahasibiwa kuwa mwenyi haki kwa ndia ya vitendo vya sharia: kwani ujuzi wa dhambi huja kwa ndia ya sharia.
- 21 Illa sasa haki ya Mwenyezi Mngu imekwisha fanywa wazi pasipokuwa na sharia, *nayo* imeshuhudiwa ni ile sharia na wale manabii:
- 22 ni ile haki ya Mwenyezi Mngu iliyo kwa ndia ya imani katika Jesu Masihi kwa wote waamninio, kwani hapana tofauti:
- 23 kwani wamefanya dhambi wote, na utukufu wa Mwenyezi Mngu hawaufikili;
- 24 ni kupawa haki bure kwa neema yakwe, kwa ndia ya ukombozi ulio katika Masihi Jesu:
- 25 ambae Mwenyezi Mngu alitangulia kumweka awe upatanisho (*makazi-ya-rehema*), kwa ndia ya imani, katika damu yakwe, illi kuonyesha haki yakwe kwa ajili ya masitahimilio, katika uvumilivu wa Mwenyezi Mngu, ya zile dhambi zilizotangulia kufanywa:

## Roehl

- 19 Lakini sisi twajua: Yote, Maonyo yanayoyasema, huwaambia wenye kuishika Maonyo, kila kinywa kifumbwe, nao ulimwengu wote uwe umepaswa na hukumu ya Mungu.
- 20 Kwa hiyo hapo, alipo, hapana mwenye mwili wa kimtu atakayepata wongofu kwa kwamba: Ameyafanya Maonyo, kwa sababu Maonyo huleta utambuzi tu wa makosa.
- 21 Lakini sasa wongofu wa Kimungu umefunuliwa pasipo Maonyo; nao unashuhudiwa na Maonyo pamoja na Wafumbaji kwamba:
- 22 Wongofu wa Kimungu ndio huu: mwanzo ni kumtegemea Yesu Kristo, nao mwisho: wote wanaomtegemea huupata. Kwani hawapitani,
- 23 kwa sababu wote wamekosa, wakalipoteza fungu lao la utukufu wa Mungu.
- 24 Kwa hiyo wanapata wongofu bure tu, kwani ni gawio, Yesu Kristo alilowapatia hapo, alipoyalipa makombozi yao.
- 25 Ndiye, Mungu aliyemtoa, kusudi wenye kumtegemea wajipatie Kiti cha Upozi katika damu yake; hapo ndipo, alipoonyesha, wongofu wake ulivyo, akiwaondolea makosa ya kale.

## Habari Njema

- 19 Tunajua kwamba sheria huwahusu walio chini ya sheria hiyo, hata hawawezi kuwa na kisingizio chochote, na ulimwengu wote uko chini ya hukumu ya Mungu.
- 20 Maana hakuna binadamu yeyote anayekubaliwa kuwa mwadilifu mbele yake Mungu kwa kushika sheria; kazi ya sheria ni kumwonyesha tu mtu kwamba ametenda dhambi.
- 21 Lakini sasa, njia ya Mungu ya kuwakubali watu kuwa waadilifu imekwisha dhihirishwa, tena bila kutegemea sheria. Sheria na manabii hushuhudia jambo hili.
- 22 Mungu huwakubali watu waadilifu kwa njia ya imani yao kwa Yesu Kristo; Mungu hufanya hivyo kwa wote wanaoamini; hakuna ubaguzi wowote.
- 23 Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa utukufu wa Mungu.
- 24 Lakini kwa zawadi ya neema ya Mungu, watu wote hukubaliwa kuwa waadilifu kwa njia ya Yesu kristo anayewakomboa.
- 25 Mungu alimtoa Yesu kusudi, kwa damu yake, awe njia ya kuwaondolea watu dhambi zao kwa imani kwake. Alifanya hivyo ili apate kuonyesha kwamba yeye ni mwadilifu. Hapo zamani Mungu alikuwa mvumilivu bila kuzijali dhambi za watu;

## **Neno**

- 19 Basi tunafahamu ya kwamba maagizo yote ya sheria ya Musa yanawahusu wale walio chini ya sheria hiyo. Kusudi la sheria ni kuwafanya watu wote wasiwe na kisingizio na kuuweka ulimwengu wote chini ya hukumu ya Mungu.
- 20 Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa kuwa na haki mbele za Mungu kwa kufuata sheria; bali sheria hatufanya tutambue dhambi.
- 21 Lakini sasa, njia ya Mungu ya kuwahesabia watu haki pasipo sheria, njia ambayo sheria na manabii huishuhudia, imekisha dhihirishwa.
- 22 Haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa kumwamini Yesu Kristo. Mungu huwatendea hivi watu wote wamwaminio Kristo pasipo kubagua,
- 23 kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;
- 24 wote wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa ukombozi ulioletwa na Yesu Kristo.
- 25 Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake. Alifanya hivi ulu kuonyesha haki yake, kwani kwa uvumilivu wake hakuziadhibu dhambi za zamani.

## **Philippians 2:5-8**

### **NRSV**

- 5 Let the same mind be in you that was in Christ Jesus,
- 6 who, though he was in the form of God, did not regard equality with God as something to be exploited,
- 7 but emptied himself, taking the form of a slave, being born in human likeness. And being found in human form,
- 8 he humbled himself and became obedient to the point of death – even death on a cross.

### **UV**

- 5 Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu;
- 6 ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho;
- 7 bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;
- 8 tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.

### **NT Zanzibar**

- 5 Maana mwe na nia hii ndani yenu iliyokuwamo na ndani ya Yesu Kristo;
- 6 yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, nae hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikamana nacho,
- 7 bali alijifanya kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wana Adamu;
- 8 tena, alipoonekana ana umbo kama mwana Adamu, alijidhili akawa mtii hatta mauti, nayo mauti ya msalaba.

#### **NT Mombasa**

- 5 Iwani na nia ii hii ndani yenu iliyokuwa ndani ya Masihi Jesu nayo:
- 6 ambac yeye alipokuwa katika sura za *mfano wa* Mngu, hakukuhasibu kufanywa sawa na Mngu kuwa ni jambo lenyi kutamaniwa,
- 7 lakini akaifanya nafusi yakwe utupu, huku akiutwaa mfano wa mtumwa, akawa sawasawa na bib-Adamu:
- 8 kisha akionekana kuwa na umbo kama wa bin-Adamu akainyenyekeza nafusi yakwe, akawa mwenyi kutii hata mauti, naam, hata mauti ya msalaba.

#### **Roehl**

- 5 Mioyoni mwenu myawaze yaleyale, Kristo Yesu aliyowaza!
- 6 Yeye alikuwa mwenye sura yake Mungu, tena kule kufanana naye Mungu hakushikamana nako kama ni kitu, alichokipokonya.
- 7 Ila alijivua mwenyewe sura ya Kimungu, akajivika sura ya kitumwa, akawa amefanana na watu; walipomtazama, akaonekana, kuwa kama mtu mwenyewe.
- 8 Akajinyenyekeza mwenyewe, akawa mwenye kutii mpaka kufa, kweli mpaka kufa msalabani.

#### **Habari Njema**

- 5 Mwe na msimamo uleule aliokuwa nao Kristo Yesu:
- 6 Yeye, kwa asili alikuwa daima Mungu; lakini hakufikiri kwamba kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kung'ang'ania kwa nguvu.
- 7 Bali, kwa hiari yake mwenyewe, aliachilia hayo yote, akajitwalia hali ya mtumishi, akawa sawa na wanaadamu, akaonekana kama wanaadamu.
- 8 Alijinyenyekeza na kutii mpaka kufa, hata kufa msalabani.

#### **Neno**

- 5 Muwe na nia kama ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu; 6 yeye kwa asili alikuwa sawa na Mungu, lakini hakuona kwamba kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikilia sana.
- 7 Bali alikubali kuacha vyote, akachukua hali ya mtumishi, akazaliwa na umbo la wanadamu.
- 8 Alipochukua umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii mpaka kufa, tena kifo cha msalaba.



**Jude 1:14**

**NRSV**

- 14 It was also about these that Enoch, in the seventh generation from Adam, prophesied, saying, "See, the Lord is coming with ten thousands of his holy ones,

**UV**

- 14 Na Henoko, mtu wa [+ kizazi cha] saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja [yuaja] na watakatifu wake, maelfu maelfu,

**NT Zanzibar**

- 14 Na Enok, wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hawo, akisema, Angalia, Bwana alikuja na elfu kumi za watakatifu wake,

**NT Mombasa**

- 14 Nae huyo Enokhu, mtu wa sabaa baada ya Adamu, aliwatolea maneno ya unabii, akisema, Huyo ndiye, Bwana alikuja pamoja na jeshi kuu mno ya watakatifu wakwe,

**Roehl**

- 14 Mambo yao aliyafumbua Henoki aliyekuwa mtu wa saba tangu Adamu, aliposema: Tazameni, Bwana anakuja pamoja na malaika zake watakatifu maelfu na maelfu,

**Habari Njema**

- 14 Naye Henoki, ambaye ni babu wa saba tangu Adamu, alibashiri hivi juu ha watu hao: "Sikilizeni! Bwana anakuja pamoja na maelfu ya malaika wake watakatifu

**Neno**

- 14 Henoki, ambaye alikuwa wa kizazi cha saba baada ya Adamu, alitoa unabii kuhusu watu hawa akasema, "Sikilizeni! Nilimwona Bwana akija na watakatifu wake maelfu kwa maelfu

## 1.2 QUR'ĀNIC PASSAGES

For each of the passages which are discussed in the study, in chapters eight, nine and ten, various Swahili versions of the Qur'ān are given as well as in English in *The Koran Interpreted* (1955) [Arberry], which is followed by: *Qurani Takatifu* [al-Farsy] (1969), as the most readily available Swahili version of the Qur'ān; *Tafsiri ya Kurani ya Kiarabu* [Dale] (1923); *Kurani Tukufu* [Aḥmadi] (1953); *Tarjuma ya AL-MUNTAKHAB katika tafsiri ya Qur'ani tukufu Qur'ani Tukufu* [Al-Barwani] (1995); *Quran Tukufu* [Mayunga] (2002); *Al-Kashif* [Mughniyya] (2002); *Juzuu ya Amma* [Al'Amin b. Aly] (1947). The final two are incomplete only the *juzuu* that have been published appear.

Note: Neither Arberry or Dale are versified. Arberry marks lines of text as a guide, Dale set his passages to be the same pagination as a readily available Arabic Qur'ān (Dale 1924:9). The Aḥmadi version includes versification of the *basmala*, meaning that the numbering of verses are one verse different from other versions.

The passages appear in the order that they appear in the Qur'ān.

### *Āl Imrān* (3):45-51

#### Arberry

- 40 When the angels said, 'Mary, God gives thee good tidings  
of a Word from Him whose name is Messiah, Jesus, son of Mary;  
high honoured shall he be in this world and the next, near stationed to God.  
He shall speak to men in the cradle, and of age, and righteousness he shall be.'  
'Lord,' said Mary, 'how shall I have a son seeing no mortal has touched me?'  
'Even so,' God said, 'God creates what He will.  
When He decrees a thing He does but say to it "Be," and it is.  
And He will teach him the Book, the Wisdom, the Torah, the Gospel,  
to be a Messenger to the Children of Israel saying, "I have come to you with a sign from  
your Lord. I will create for you out of clay as the likeness of a bird;  
then I will breathe into it, and it will be a bird, by the leave of God.  
I will also heal the blind and the leper, and bring to life the dead, by the leave of God.  
I will inform you too of what things you eat, and what you treasure up in your houses.  
Surely in that is a sign for you, if you are believers.  
Likewise confirming the truth of the Torah that is before me,  
and to make lawful to you certain things that before were forbidden unto you.  
I have come to you with a sign from your Lord;  
so fear you God, and obey you me.  
Surely God is my Lord and your Lord;  
so serve Him. This is a straight path".'

### Al Farsy

- 45 (Kumbukeni) waliposema Malaika: “Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kumzaa mtoto bila ya mume, bali kwa kutamkwa) Neno tu litokalo Kwake (la kukwambia ‘Zaa’ ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masihi, Isa, mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu.
- 46 “Naye atazungumza na watu (maneno ya dini) katika utoto (wake) na katika utuuzima (wake), na (atakuwa) katika watu wema (kabisa).”
- 47 (Maryamu) akasema: “Mola wangu! Nitapataje mtoto, na hali ya mtu yoyote hakunigusa?” Akasema (Mola wake): “Ndivyo vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu huumba Anavyopenda: Anapohukumu jambo, Huliambia: ‘Kuwa’, (basi) likawa.
- 48 “Na (Mwenyezi Mungu) atamfunza kuandika na kujua ilimu na (kujua) Taurati na Injili.
- 49 “Na (Atamfanya) Mtume kwa wana wa Israili, (kuwaambia): ‘Nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nakuumbieni, katika udongo, kama sura ya ndege, kisha nampuliza, mara anakuwa ndege, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponyesha vipofu na wenye mabalanga, na ninawafufua (baadhi ya) waliokufa, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na nitakwambieni mtakavyovila na mtakavyo weka akiba katika nyumba zenu. Bila shaka katika haya imo hoja kwenu ikiwa nyinyi ni watu wa kuamini!
- 50 “Na (nitakuwa) msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu kabla yangu katika Taurati; na (nimekuja) ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa, na nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini.
- 51 “Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabudini. Hii ndiyo njia iliyonyooka.”

### Dale

Malaika aliposema, Ee Maryamu, hakika yake Mungu anakubashiria khabari za Neno litokalo kwake, jina lake Masihi Isa bin Maryamu, mtukufu katika dunia na Akhera, na mmoja wao ambao mahali pao ni karibu na Mungu, nae atasema na watu akiwa katika kitanda cha mtoto, na atakapokuwa mtu mzima, nae atakuwa mmoja wao wenye haki. Akasema, Bwana wangu, nitawezaje kuwa na mtoto ikiwa mwana Adamu hajanigusa? Akasema, Kadhalika, Mungu hukhuluku atakacho. Akikusudia kutenda neno husema tu, Liwe likawa; nae atamfundisha kitabu na hekima na Torati na Injili; nae atakuwa mtume kwa watu wa Israeli, akisema, kwamba, Nimekuja kwenu na ishara itokayo kwa Mungu, yaani nitawakhulukieni kwa udongo kitu kana kwamba kina mfano wa ndege, nami nitakipulizia, nacho kitakuwa ndege kwa idhini ya Mungu; nami nitamponya mtu aliyezaliwa kipofu, na mwenye ukoma; nami nitawahuisa waliokufa, kwa idhini ya Mungu; nami nitawaambieni mnachokula, nacho mnachoweka akiba nyumbani mwenu. Hakika yake katika hayo iko ishara kwenu, ikiwa mnaamini.

Nami nitaithubutisha Torati mliyo nayo, na yakini nitawahalalishieni baadhi ya vitu vilivyokuwa haramu kwenu. Nimekuja kwenu na ishara itokayo kwa Bwana wenu; bassi mcheni Mungu mkanifuata; mwabuduni yeye: hii ndiyo njia iliyonyoka.

#### Aḥmadi

- 46 (Kumbukeni) waliposema Malaika: Ewe Mariamu, bila shaka Mwenyezi Mungu Anakupa habari njema za neno litokalo Kwake, jina lake Masihi Isa mwana wa Mariamu, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu miongoni mwa waliokaribishwa.
- 47 Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima, na atakuwa katika watu wema.
- 48 (Mariamu) akasema: Mola wangu, nitampataje mtoto na hali mtu ye yote hakunigusa? Akasema: hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Huumba Anavyopenda: Anapohukumu jambo, basi Huliambia tu, Kuwa, basi huwa.
- 49 Na (Mwenyezi Mungu) Atamfunza Kitabu na hekima na Taurati na Injili.
- 50 Na (Atamfanya) Mtume kwa wana wa Israeli, (kuwaambia), Nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nawaumbieni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege, kisha napulizia ndani yake, mara huwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninamponya kipofu na mwenye ukoma, na kuwahuisha wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninawaumbieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu; bila shaka katika hayo imo Ishara kwenu ikiwa ninyi mnaamini.
- 51 Na msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ili niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa, na nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, kwa hiyo Mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini.
- 52 Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu, basi Mwabuduni; hii ndiyo njia iliyonyoka.

#### Al-Barwani

- 45 Na pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa walio karibishwa (kwa Mwenyezi Mungu).
- 46 Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema.
- 47 Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba apendacho. Anapo hukumu jambo, huliambia: Kuwa! Likawa.
- 48 Na atamfunza kuandika na Hikima na Taurati na Injili.
- 49 Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini.
- 50 Na ninasadikisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlio harimishiwa, na nimekujieni na Ishara kutokana na Mole Mlezi weni. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi.
- 51 Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabudni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.

### Mayunga

- 45 (Kumbukeni) Malaika waliposema: Ewe Mariam! Hakika Mwenyeezi Mungu anakupa khabari njema za neno litokalo kwake, jina lake ni Masihi Isa Mwana wa Mariam, mwenye heshima ulimwenguni na Akhera, na ni miongoni mwa wenye kukurubishwa (mbele ya Mwenyeezi Mungu).
- 46 Atasema na watu katika uchanga na utu uzima, na atakuwa katika watu wema.
- 47 Akasema (Mariam): Mola wangu! nitampataje mtoto na hali mtu yeyote hakunigusa? Akasema: Hivyo ndivyo Mwenyeezi Mungu huumba anavyotaka, anapohukumu jambo basi huliambia kuwa basi huwa.
- 48 Na (Mwenyeezi Mungu) atamfundisha kuandika na (kujua) elimu na (kujua) Taurati na Injili.
- 49 Na (atamfanya) Mtume kwa wana wa Israel, (awaambie) Hakika mimi nimewajieni na dalili itokayo kwa Mola wenu. Mimi nitakufanyieni katika udongo kama namna ya ndege, kisha napulizia ndani yake (awe) ni ndege kwa idhini ya Mwenyeezi Mungu. Na niwapoze vipofu na wenye mbalanga, niwafufue wafu kwa idhini ya Mwenyeezi Mungu. Na niwape khabari na mnavyokula na mnavyoviweka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika hayo mna dalili kwenu ikiwa nyinyi ni wenye kuamini.
- 50 Na ninasadikisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati na ili niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharamishiwa. Na nimewajieni na dalili kutoka kwa Mola wenu, basi Mcheni Mwenyeezi Mungu na nitiini.
- 51 Hakika Mwenyeezi Mungu ndiye Mola wangu na ni Mola wenu, basi muabuduni, hii ndiyo njia iliyonyooka.

### Mughniyya

- 45 Waliposema Malaika: Ewe Maryam! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria neno litokalo kwake; jina lake ni Masih mwana wa Maryam; mwenye heshima duniani na akhera na ni miongoni mwa waliokurubishwa.
- 46 Na atasema na watu katika uchanga na katika utu uzima na atakuwa miongoni mwa watu wema.
- 47 Akasema: “Mola wangu! Nitakuwaje na mtoto na hali hajanigusa mtu yeyote?” Akasema: Ndivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba anavyotaka anapohukumu jambo, huliambia ‘kuwa’ likawa.
- 48 Na atamfundisha kuandika na hekima na Tawrat na Injili.
- 49 Na Mtume kwa wana wa Israil. Mimi nimewajia na Ishara kutoka kwa Mola wenu, hakika mimi nitawafanyia kama namna ya ndege katika udongo; kasha nimpulizie awe ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na niwaponye vipofu na wenye mbalanga. Niwafufue wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na niwaambie mnavyovila na mtakavyoweka akiba. Hakika katika haya ipo ishara kwenu mkiwa ni wenye kuamini.
- 50 Na msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Tawrat, na ili niwahalalishie baadhi ya mliyoharamishiwana nimewajia na ishara kutoka kwa Mola wenu, kwa hiyo mcheni Mwenyezi Mungu na mtiini.
- 51 Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka.

***Al-Nisā'* (4):157-159**

**Arberry**

And for their saying, 'We slew the Messiah,  
Jesus son of Mary, the Messenger of God' –  
yet they did not slay him, neither crucified him,  
only a likeness of that was shown to them.  
Those who are at variance concerning him surely  
are in doubt regarding him; they have no knowledge  
of him, except the following of surmise;  
and they slew him not of a certainty –  
no indeed; God raised him up to Him; God is  
All-mighty, All-wise.  
There is not one of the People of the Book  
but will assuredly believe in him before his  
death, and on the Resurrection Day he will be  
a witness against them.

**Al-Farsy**

- 157 Na kwa (ajili ya) kusema kwao: “Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mungu,” hali hawakumwua wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwengine wakamdhani Nabii Isa). Na kwa hakika wale waliokhitalifiana katika (hakika) hiyo (ya kumwua Nabii Isa) wamo katika shaka nalo (jambo hilo la kusema kauawa). Wao (kabisa) hawana yakini juu ya (jambo) hili (la kuwa kweli wamemwua Nabii Isa), isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumwua.
- 158 Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua Kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.
- 159 Na hakuna yoyote katika watu waliopewa Kitabu (Mayahudi an Manasara) ila humwamini (Nabii Isa kwa hakika yake) kabla ya kifo cha kila mmoja katika hao. (Lakini hakuna faida kumwamini huko wakati huo). Naye (Masihi) Siku ya Kiama atakuwa shahidi juu yao.

**Dale**

[N]a kusema, Hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Maryamu, mtume wa Mungu; nao hawakumwua wala hawakumsulubi walakini walipewa mtu aliyefananishwa nae; na hakika wale waliokhitalifiana katika khabari zake walikuwa hali ya mashaka juu ya hayo, wala hawakuwa na elimu; walifuata dhana tu. Hawakumwua kweli kweli: bali Mungu alimrafaisha awe karibu nae, na Mungu ni mwenye uweza, mwenye hekima. Hapatakuwa mtu mmoja katika watu wa kitabu asiyemwamini kabla ya mauti yake: na siku ya kiyama atakuwa shahidi juu yao.

### **Aḥmadi**

- 158 Na kusema kwao: Hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumwua –
- 159 Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye Hekima.
- 160 Na hakuna ye yote katika watu wa Kitabu ila ataliadini kabla ya kifo chake, naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

### **Al-Barwani**

- 157 Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu – nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitilafiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini.
- 158 Bali Mwenyezi Mungu alimtukuza kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.
- 159 Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuadini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

### **Mayunga**

- 157 Na kusema kwao Hakika tumemuuwa Masihi Isa mwana wa Mariam, Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala hawakumuuwa wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa kwao. Na hakika ambao wamekhitilafiana katika khabari yake wana shaka nayo, hawana ujuzi wowote ila kufuata dhana tu, wala hawakumuuwa kwa yakini.
- 158 Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.
- 159 Na hakuna yeyote katika watu wa Kitabu ila humwamini yeye (Isa) kabla ya kufa kwake, na siku ya Kiyama atakuwa (Isa) shahidi juu yao.

### **Mughniyya**

- 157 Na kwa kusema kwao: sisi tumemuuwa Masih Isa, mwana wa Maryam Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na hawakumuuwa wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa kwao. Na hakika wale waliohitilafiana katika haya wamo katika shaka nayo; hawana ujuzi ila kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini.
- 158 Bali Mwenyezi Mungu alimwinua kwake, na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hekima.
- 159 Na hakuna katika watu wa Kitabu ila humwamini yeye kabla ya kufa kwake, na Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

***Al-Nisā'* (4):171**

**Arberry**

People of the Book, go not beyond the bounds  
of your religion, and say not as to God  
but the truth. The Messiah, Jesus son of Mary,  
was only the Messenger of God, and His Word  
that He committed to Mary, and a Spirit from  
Him. So believe in God and His Messengers,  
and say not, 'Three.' Refrain; better is it  
for you. God is only One God. Glory be  
to Him – that He should have a son!  
To Him belongs all that is in the heavens  
and in the earth; God suffices  
for a guardian.

**Al Farsy**

171 Enyi watu wa Kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli. Masihi Isa bin Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na (ni kiumbe aliyeumbwa kwa) tamko Lake (tu Mwenyezi Mungu) alilompelekea Maryamu. Na ni roho iliyotoka Kwake (Mwenyezi Mungu kama roho nyengine). Basi mwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Yake; wala msiseme “watatu ...” Jizueni (na itikadi hiyo); itakuwa bora kwenu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na Utakatifu Wake kuwa ana mwana. Ni Vyake (vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa kutosha.

**Dale**

Enyi watu wa kitabu, msiruke mipaka katika dini yenu, wala msiseme khabari za Mungu illa za kweli. Hakika Isa Masihi bin Maryamu ni mtume wa Mungu, na Neno lake alilomtia katika Maryamu; ni Roho itokayo kwake; mwaminini Mungu bassi, na mitume wake: wala msiseme, Watatu; acheni kusema hivi; itakuwa kheri zaidi kwenu. Mungu ni Mungu mmoja; haikumlaiki awe na mwana: vitu vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani ni mali yake; na Mungu atosheleza kuwa mtunzaji.

**Aḥmadi**

172 Enyi watu wa Kitabu! msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli: Masihi Isa bin Mariamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno Lake tu Alilompelekea Mariamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake; wala msiseme watatu, jizuieni, itakuwa bora kwenu; bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu Wake ya kwamba Awe na mwana. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mlinzi.



### **Al-Barwani**

171 Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lilio kweli. Hakika Masihi Isa mwana wa Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na neno lake tu alilo mpelekea Maryamu, na ni roho iliyo toka kwake. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Wala msiseme: Utatu. Komeni! Itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu. Ametukuka Yeye vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.

### **Mayunga**

171 Enyi watu wa Kitabu! msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila lililo kweli. Hakika Masihi Isa mwana wa Mariam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni neno lake tu alimpelekea Mariam, na ni roho itokayo kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake, wala msiseme watatu, wacheni (itikadi hiyo) ni bora kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu, ameepekana na kuwa na mtoto. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mlinzi,

### **Mughniyya**

171 Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki. Masihi Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam, na ni roho iliyotoka kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume wake; wala msiseme watatu. Komeni!, itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu. Ameepekana kuwa na mtoto. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi.

*Al-Mā'ida (5):72-78*

**Arberry**

They are unbelievers who say, 'God is the Messiah, Mary's son.'  
For the Messiah said, 'Children of Israel, serve God, my Lord and your Lord.  
Verily whoso associates with God anything,  
God shall prohibit him entrance to Paradise, and his refuge shall be the Fire;  
and wrongdoers shall have no helpers.'

They are unbelievers who say, 'God is the Third of Three.'  
No God is there but One God. If they refrain not from what they say,  
there shall afflict those of them that disbelieve a painful chastisement.  
Will they not turn to God and pray His forgiveness?  
God is All-forgiving, All-compassionate.

The Messiah, son of Mary, was only a Messenger;  
Messengers before him passed away; his mother was a just woman;  
they both ate food. Behold, how We make clear signs to them;  
then behold, how they perverted are!

- 80 Say: 'Do you serve, apart from God, that which cannot hurt or profit you?  
God is the All-hearing, the All-knowing.'  
Say: 'People of the Book, go not beyond the bounds in your religion,  
other than the truth, and follow not the caprices of a people who went astray before,  
and led astray many, and now again have gone astray from the right way.  
Cursed were the unbelievers of the Children of Israel by the tongue of David,  
and Jesus, Mary's son; that, for their rebelling and their transgression.

### Al-Farsy

- 72 Bila ya shaka wamekufuru wale waliosema, “Mwenyezi Mungu ni Masihi (Isa) bin Maryamu.” Na (hali ya kuwa) Masihi alisema: “Enyi wana wa Israili! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahali pake (patakuwa) ni Motoni na madhalimu hawatakuwa na wasaidizi (wa kuwasaidia Siku ya Kiama).”
- 73 Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: “Mwenyezi Mungu ni Mmoja katika (wale waungu) watatu; (Yeye ndiye wa tatu wao).” Hali hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu Mmoja (tu peke yake). Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa yakini itawakamata – wale wanaoendelea na ukafiri miongoni mwao – adhabu iumizayo.
- 74 Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.
- 75 Masihi bin Maryamu si chochote ila ni Mtume (tu). (Na) bila shaka Mitume wengi wamepita kabla yake. (Hawajaona)? Na mamake ni mwanamke mkweli. (Na) wote wawili walikuwa wakila chakula (na wakenda choo. Basi waungu gani wanaokula na kwenda choo)? Tazama jinsi Tunavyobainishia Aya, kisha tazama jinsi wanavyogeuzwa (kuacha haki).
- 76 Sema: “Je! Mnawaabudu – badala ya Mwenyezi Mungu (peke yake) – wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukunufaisheni? Na Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye (na) ndiye Ajuaye.”
- 77 Sema: “Enyi watu wa Kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu bila haki, wala msifuate matamano ya watu waliokwisha potea toka zamani; (nao ndio hao wanavyuoni wenu) na wakawapoteza wengi, na (sasa) wanapotea njia iliyo sawa, (hawataki kumfuata Nabii Muhammad).”
- 78 Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israili kwa ulimi wa Daudi na wa Isa bin Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakipindukia mipaka (sana).

### Dale

Bila shaka watu wale wasemao ya kuwa Mungu ni Masihi mwana wa Mariamu wamekufuru: kwa maana Masihi alisema, Enyi wana wa Israeli, mwabuduni Mungu, Bwana wangu na Bwana wenu: mtu aliye yote atakaempa Mungu mshirika, Mungu atamharamishia Bustani, na moto utakuwa kao lake, wala hapana wasaidizi kwao wenye kudhulumu. Wao wasemao ya kuwa Mungu ni wa tatu wa watatu wamekwisha kukufuru. Hapana Mungu illa Mungu mmoja; nao wasipoacha kusema wasemavyo, hakika yake adhabu kali itawapata wale miongoni mwao walio makafiri. Je! hawatatubu na kumwelekea Mungu na kumwomba ghofira? Maana Mungu ni mwenye ghofira na mwenye rehema. Masihi, mwana wa Mariamu,

ni mtume tu, mitume wengine wameantangulia: na mama yake alikuwa msema kweli: wote wawili walikula chakula. Tazama jinsi tunavyowadhihirishia ishara zetu: kiisha tazama jinsi wanavyogeuka upande. Sema, Je! mnataka kuabudu pamoja na Mungu kitu kisichoweza kudhuru wala kusaidia? Lakini Mungu anasikia, anajua.

Sema, Enyi watu wa Kitabu, msiruke mipaka ya kweli katika dini yenu: wala msifuate tamaa zao waliokwisha kupotea, waliowakosesha watu wengi; nao wenyewe wamepotea mabli ya njia iliyo sawa sawa.

Watu wale miongoni mwa wana wa Israeli wasioamini walilaamiwa kwa kinywa cha Daud, na cha Isa bin Mariamu. Haya yalikuwa kwa sababu waliasi wakawa wakaidi.

### Aḥmadi

